THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/1

**KISWAHILI 1**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

*Muda: Saa 3* **2006 Februari, 06 Jumatatu Mchana**

---

*MAELEZO*

1. Karatasi hii ina maswali **kumi na tatu** (13) katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano** (5) kwa kuchagua swali moja kutoka kila sehemu.
3. Simu za mikononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A : HISTORIA (alama 20)

1. "Serikali baada ya uhuru ilijitahidi sana katika kukuza Kiswahili nchini Tanzania". Thibitisha kauli hiyo kwa kutoa mifano dhahiri.

2. Jadili sababu za Kiswahili kuwa lugha ya Taifa nchini Tanzania kuliko lugha nyingine za Kibantu.

3. "Kiswahili kilianzia Kongo kikaenea hadi Pwani ya Afrika Mashariki". Kubali au kataa usemi huo kwa kutoa hoja za Historia ya Kiswahili.

## SEHEMU B : SARUFI (alama 20)

4. Kwa kutoa mifano onesha aina za nomino. Je, uainishaji huo una dosari gani?

5. "Umbo la kitenzi huundwa na vipashio mbalimbali vinavyobeba dhima mbalimbali". Thibitisha kauli hiyo kwa kutumia vitenzi vifuatavyo:

   (a) Anakunywa.

   (b) Mnasali.

   (c) Tunamshukuru.

   (d) Watalia.

6. Onesha kwa kupigia mstari mofimu - Ki- kuweza kuwa na dhima zifuatazo.

   (a) - Ki - kuunda mzizi wa neno.

   (b) - Ki - kuonesha mtendwa jambo.

   (c) - Ki - kuonesha upatanisho wa kisarufi.

   (d) - Ki - kushurtisha

## SEHEMU C : MATUMIZI (alama 20)

7. "Watanzania ni watumiaji wa Kiswahili na wakikosa nafasi hiyo madhara yake ni makubwa". Kwa kutoa mifano eleza ni madhara gani yanayoweza kujitokeza?

8. Ukitumia mfano wa sentensi kwa kila tumizi onesha matumizi matano ya kiunganishi "kwa".

9. Kwa kutoa mfano wa sentensi kwa kila tumizi eleza matumizi matano ya neno "pamba"

## SEHEMU D : UTUNGAJI (alama 20)

10. Andika risala kwa niaba ya wanafunzi wenzako kwa mgeni mwalikwa katika mahafali yenu ya kumaliza kidato cha 6.

11. Andika insha ya maneno yasiyopungua 300 na yasiyozidi 400 juu ya Mgaa gaa na upwa hali wali mkavu.

12. Andika barua katika gazeti la "Mwananchi" kuhusu kero ya ubovu wa barabara zinazounganisha wilaya unayoishi. Jina lako ni Ari Mpya, S.L.P 4030, Kilomeni Mwanga.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU E : UFAHAMU (alama 20)

11. Soma habari hii kisha jibu maswali yanayofuata:

Ndani, kama nilivyosema, kiza totoro! Hapana mmoja aliyemwona mwenziwe. Kunatisha! Kama asingeogopa kuambiwa mwoga, angeghairi kwenda mbele. Si mahali pa kupita mtu. Vimulimuli vimetawanyika husema usiku wa manane, vinang'ara kama nyota za usiku usiotoka mbalamwezi, ila "nyota" zile za mzimuni zilikuwa zinang'ara, kwa wakati ule, mchana, na zinazunguka huko na huko ndani ya mzimu, na wakati mwingine zilitaka hata kuingia katika macho ya wavulana wetu wawili majasiri. Kwa hiyo haistaajabishi, tukiona kuwa mwendo wao ulikuwa wa kutayamamu, wanapita na huku wanavikupua vile vimulimuli vilivyokuwa vinawajia usoni kila mara. Popo vilevile walikuwa wanaruka na kuwapigia mbawa zao usoni, kelele za komba na mabundi, walikuwa hawana habari kama kumekucha zilikuwa zikiwazomea mwote walimokuwa wakipita.

Kwa mbali, inapata pima mia moja waliona baka moja jeupe lililotawanyika na kuchukuwa nafasi kubwa kidogo, na waliweza kukisia kuwa lile lilikuwa baka la jua, lakini kwa huku waliko halikufika hata kidogo anga lake.

Hapana aliyesema neno, wote wawili walikuwa wakienda kama mabubu.

Baada ya kitambo, vimulimuli vilianza kupungua, na mwendo wao, ingawa hado kiza, lakini ulikuwa haujambo kidogo. Walipoanza kulikaribia lile anga la jua, hata kiza nacho kilianza kukimbia kidogo kidogo.

Walipofika kunapo lile anga la jua, waliona kuwa sehemu ile ya kichaka ilikuwa kidogo imetanzuka, kwa sababu miti ilipungua kuambatana; hapo walisimama kupumzika. Iliwachukua safari ya kiasi cha nusu saa hata wakafika pale. Alitia kidole katika tundu la mtemba wake, na alipokitoa, alikung'uta jivu juu ya kiatu chake, akapuliza kwa nguvu kuzidi kusafisha, kisha akatia mnoga wake, akawasha kiberiti, upepo ulikuwa shwari, na moshi wote ulitanda hewani kwa muda kabla haujatanzuka, na harufu ya mnoga wake ilitosha kuwa bahari ya kuufikiza "Mzimu wa Watu wa Kale".

Baada ya kuvuta mara tatu nne, waliendelea na safari yao, sasa bila ya taabu kubwa; kwa hiyo, sasa ndiyo kwanza kila mmoja alitafuta ulimi wake ulikokwenda. Mmoja aliuliza, "Mtu akikaa kimya na kuchorachora upuuzi tu, anachora kitu cha maana au kitu cha upuuzi tu vile vile?" Lakini sauti yake alivyokuwa akisema bila ya kumtupia jicho sahibu yake, alionesha kuwa anasema na nafsi yake tu kwa sauti. Kwa hakika hakutaraji jawabu la swali hili kwa yule mwenziye maana mara aliendelea mwenyewe kwa mwenyewe, ila sasa aligeuka kumtazama mwenziwe usoni, "zipo sababu mbili zitakazokuzuia, rafiki yangu, kuniambia kwamba maneno yale yaliyoandikwa kwa Kiarabu katika karatasi ile ya Bwana Ali hayakuwa na maana kwa mwenyewe aliyeandika". Aliendelea kuvuta kiko chake kwanza akimwacha Najum yamwingie barabara maneno yake aliyoyasema. Halafu akaendelea, "Moja katika sababu hizo ni hii, kuandika stakabadhi ya mali mwenyewe, tena akawa nayo mwenyewe, asimpe mtu aliyemwuzia. Sababu ya pili hakutia sahihi yake wala tarehe alipoandika karatasi ile. Mambo mawili haya yatakuonesha dhahiri kuwa ile karatasi ni kitu muhimu sana, wala haionesh kuwa Bwana Ali alikuwa kakaa kitako bila kazi akawa anachora tu".

Najum alitazama akaona sasa Bwana Msa anasema maneno ya upuuzi; maana mambo mawili hayo aliyoyataja yanapingana yenyewe kwa yenyewe na yanarejea kule kuwa karatasi ile ni upuzi tu. Ikiwa ile ni stakabadhi hakika, basi yule Banyani alikuwa mpumbavu asiipokee kwa Bwana Ali akawa nayo mwenyewe. Na vile vile ilivyokuwa stakabadhi yenyewe haina sahihi wala tarehe, basi inafuta yale masala ya hakika yake, na kuifanya stakabadhi ile vile vile ni upuzi tu. Kinyume cha mambo, leo, inaonesha dhahiri kuwa Bwana Msa ana wazimu!



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Najum hakuwahi kusema neno, na mara Bwana Msa alianza kusema, "Achilia mbali hayo; unakumbuka tumesikia kuwa Bwana Ali anatafuta mshtiri wa mali yake kwa upesi na tena kwamba alionekana anamkaguza Seti mali yake yote? Ukiyatia hayo roboni, utaona kuwa ni muhali kwa Bwana Ali kukaa kitako hali hana kazi ila kuchora mkataba wa stakabadhi ya mapesa si kidogo bure bure tu; lazima alikuwa na dhamiri fulani katika akili yake hata akakaa kuchora stakabadhi ile".

**MASWALI:**

(a) Toa maana ya maneno yafuatayo:

(i) Totoro
(ii) Wanavikupua
(iii) Haistajabishi
(iv) Pima
(v) Kutayamamu
(vi) Mnoga
(vii) Buhuri
(viii) Kila mmoja alitafuta ulimi wake ulikokwenda
(ix) Dhamiri
(x) Anakaguza.

(b) Mwandishi anasema hali ya mzimu wa watu wa kale ikoje?

(c) Kwa nini mwandishi anasema hawa vijana wawili ni mashujaa?

(d) Upuzi wa Bwana Msa ni upi? Na upuzi wa stakabadhi ni upi?

(e) Andika ufupisho usiopungua maneno 150 na usiozidi maneno 250.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org